

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



TAARIFA KWA UMMA

Desemba 21, 2022

www.ludewadc.go.tz

LUDEWA, NJOMBE- TANZANIA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratia leo Desemba 21, 2022 amepokea wawekezaji kutoka Jijini Dar es Salaam waliokuja kwa ajili ya kujitambulisha na kubainisha uwekezaji wanaohitaji kuwekeza ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Kampuni ya **A1000 ZARA INVESTMENT** yenye makao makuu yake Jijini Dar es Salaam inayojishughulisha na shughuli mbalimbali hapa nchini Tanzania ikiwa ni pamoja na Kilimo imeomba shamba lenye ukubwa wa ekali 750 ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Wilaya ya Ludewa ili kufanya uwekezaji wa uzalishaji wa Mbegu za mazao ya Mahindi na Maharage pamoja na uzalishaji wa mahindi lishe kwa ajili ya chakula.

Mkurugenzi wa Kampuni hiyo Bw. Joseph John Mwema amesema, Ujio wake ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ni kufanya uwekezaji katika mazao tofauti ila kwa sasa atajikita katika Kilimo cha mahindi na maharage kwenye eneo la bonde la umwagiliaji katika kijiji cha Lifua ambapo anatarajia mara baada taratibu zote za kisheria kukamilika kuanza uwekezaji huo mapema Januari, 2023.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday amewapokea na kusema kuwa, "Serikali ipo tayari kutoa ushirikiano kwa wawekezaji wote wanaokuja kuwekeza ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, natumia nafasi hii kuwakaribisha Ludewa Wilaya yenye utajiri mkubwa wa maeneo ya uwekezaji wa shughuli za Kilimo. Pia nawaombe mara baada ya kusaini mkataba wa uwekezaji wenu muwatumie wananchi wa Wilaya ya Ludewa kwa kuwapa fursa ya ajira kwani hao ndio walenzi wa maeneo hayo na iwe sehemu ya darasa kwa wakulima wanaozunguka maeneo ya mradi huo ili wawe wanufaika na uwekezaji wenu Karibuni sana".

Chrispin B. Kalinga

Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini